

Na Rais Thomas S. Monson

# Amefufuka!

*Kaburi tupu asubuhi hiyo ya Pasaka ya Kwanza ilikuwa jibu kwa swali la Ayubu, "Kama mtu akifa, ataishi tena?"*

Hiki kimekuwa ni kikao cha kufana sana. Kwa niaba ya wale wote walioshiriki mpaka sasa kwa kunena au nyimbo, kama Rais wa Kanisa, nimechagua kusema kwenu kwa wepesi hivi sasa maneno mawili tu, yanayojulikana kama maneno mawili muhimu sana katika lugha ya Kiingereza. Kwa Dada Cheryl Lant na washauri wake, kwaya, wacheza muziki, wasemaji, maneno hayo ni "Asanteni."

Miaka mingi iliyopita, nikiwa London, Uiingereza, nilitembelea nyumba ya sanaa maarufu inayojulikana kama Tate. Kazi za Gainsborough, Rembrandt, Constable na wasanii wengine mashuhuri zilikuwa zinaonyeshwa katika chumba baada ya chumba. Nilifurahishwa na umaridadi wao na nikatambua ujuzi ambao ulihitajika kutengeneza hizi kazi bora. Kilichowekwa kando kwenye pembe tulivu katika rafu ya tatu, hata hivyo, ulikuwa ni mchoro ambao sio tu uliovutia mawazo yangu bali pia ulinasa moyo wangu. Mchoraji, Frank Bramley, alikuwa amechora nyumba ndogo duni uliyoangalia bahari iliyozolewa na upepo. Wanawake wawili, mama na mke mvuvi asiyekuwepo, walikuwa wametazama na wamengojea usiku kucha kurudi kwake. Sasa usiku ulikuwa umepita, ukweli ulikuwa umetokea kwamba alikuwa amepotelea baharini na hangerudi. Akipiga magoti kando ya mama mkwe wake, kichwa kimezikwa kwenye paja la huyu mama mzee, mke kijana alikuwa analia kwa kutamauka. Mshumaa ulioisha kwenye ubao wa dirisha hunena kuhusu mkesha usio na matunda.

Nilihisi kusononeka kwa huyu mwanamke kijana; nilihisi huzuni yake. Maandishi kwa maringo ambayo mchoraji alikuwa amepatia hii kazi yake yalisimulia hadithi ya kuhuzunisha. Yalisomeka: Ucheo usio na Matumaini.

Ee, jinsi gani huyu mwanamke kijana alitamani faraja, hata uhalisi, wa "Misa ya Wafu" ya Robert Louis Stevenson:

*Baharia yu nyumbani, nyumbani*
*mbali na bahari*
*Na mwindaji, nyumbani mbali*
*na mlima.*[1]

Miongoni mwa kweli zote za maisha ya kimwili, hakuna ilio yakini kabisa kama mwisho wake. Kifo huja kwa wote; ni "urithi wetu sote. Kinaweza kuwadai mhathiriwa wake katika uchanga au ujana; [kinaweza kutembelea] katika wakati maisha yapo kileleni; au kuita kwake kunaweza kuahirishwa mpaka theluji ya miaka imekushanyika juu ya . . . kichwa; kinaweza kuja kama matokeo ya ajali au ugonjwa, . . . au . . . kupitia kwa mambo ya halisi; lakini kuja ni lazima."[2] Pasipo kuepukika kinawakilisha uchungu wa kupoteza uhusiano na, hasa katika ujana, pigo la kuvunjwa kwa ndoto ambazo hazijatimizika, malengo ambayo hayajafikiwa na matumaini yaliyotiishwa.

Kile gani kiumbe hai, kinachokabiliana na kupoteza mpendwa wake au hakika, kusimama mwenyewe kwenye mwisho wa pasipo kikomo, hakijatafakari kile kilicho nyuma ya pazia ambayo kinatenganisha yanayoonekana na yasiyoonekana?

Karne zilizopita, mtu Ayubu—ambaye alikuwa amebarikiwa na kila aina ya kipawa cha mali, ila tu kujipata mwenyewe kuumizwa na yote ambayo yanaweza kumtokea mwanadamu—alikaa na wenziwe na kutamka swali, lisilo la wakati na uzee,

"Kama mtu akifa, angeishi tena?"[3] Ayubu aliongea kile kila mwanaume na mwanamke ameshatafakari.

Asubuhi hii tukufu ya Pasaka ningependa kuliangalia swali la Ayubu—"Kama mtu akifa, angeishi tena?"—na kutoa jibu ambalo linatokana sio tu kwenye kuangalia kimawazo bali pia kutoka kwenye neno lililofunuliwa la Mungu. Ninaanza na yale ya muhimu.

Kama kuna usanifu katika ulimwengu huu ambamo tunaishi, lazima kuna Msanifu. Ni nani anayeweza kuyaoana maajabu mengi ya mifumo ya sayari bila kuamini kwamba kuna usanifu kwa wanadamu wote. Nani anaweza kushuku kuwa kuna Msanifu?

Katika kitabu cha Mwanzo tunajifunza kwamba Msanifu Mkuu aliumba mbingu na nchi. "Na nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji."

"Iwe nuru," alisema yule Msanifu Mkuu, "na ikawa nuru." Akaumba anga. Akatenganisha nchi na maji na kusema, "Nchi itoe majani, . . . mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake."

Mianga miwili aliiumba—jua na mwezi. Zikaja nyota kwa usanifu Wake. Aliwaita viumba hai katika maji na ndege wanaopaa juu ya nchi. Na ikawa hivyo. Aliumba mifugo, wanyama, na vile vya kutambaa. Usanifu ukakamilika.

Mwisho wa wote, Alimuumba mtu kwa mfano Wake—mume na mke—watawale juu ya viumbe vile vingine vyote.[4]

Mtu peke yake ndiye aliyepokea akili—ubongo, fikra, na nafsi. Mtu pekee, akiwa na hizi sifa, alikuwa na uwezo wa imani na matumaini, kwa maongozi na tamaa.

Nani anayeweza kubishana kwa ushawishi kwamba mtu—kazi tukufu ya Msanifu Mkuu, akiwa na utawala juu ya viumbe hai vyote, akiwa na ubongo, na upendeleo, na fikra na nafsi, na akili na utukufu, anafaa kufikia mwisho wakati roho inapoiacha hekalu la udongo?

Ili kufahamu maana ya kifo, lazima tuelewe madhumuni ya uzima. Nuru ififiao ya imani ni lazima iwe chini ya jua la mchana wa ufunuo, kwa ambayo kwayo tunajua tuliishi kabla ya kuzaliwa kwetu kimwili. Katika hali yetu kabla kuzaliwa, bila shaka tulikuwa miongoni mwa wana na mabinti wa Mungu waliopaza sauti kwa shangwe kwa sababu ya nafasi ya kuja kwenye hii hali ya kuishi kimwili yenye changamoto.[5] Tunajua madhumuni yetu ilikuwa ni kupata mwili, na kushinda majaribu na kudhibitisha kwamba tutaweka amri za Mungu. Baba yetu wa Mbinguni alijua kwa sababu za uhalisi wa maisha ya kimwili, tutajaribiwa, tutatenda dhambi, na tutakosa kufikia kiwango. Ili tupate kila nafasi ya ufanisi, Alimweka Mwokozi ambaye angeteseka na kufa kwa ajili yetu. Si tu angefanya upatanisho kwa dhambi zetu, bali kama sehemu ya upatanisho huu pia angeshinda kifo cha mwili ambacho sote tuko chini yake kwa sababu ya Anguko la Adamu.

Kwa hivyo, zaidi ya miaka 2,000 iliopita, Kristo, Mwokozi wetu alizaliwa katika maisha ya kimwili katika zizi katika Bethlehemu. Masiya aliyetabiriwa akaja.

Kuna machache sana yaliyoandikwa kuhusu uvulana wa Yesu. Napenda ujumbe kutoka Luka: "Na Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu."[6] Na kutoka kwa kitabu cha Matendo ya Mitume, kuna mstari mfupi kuhusu Mwokozi ambao una maana nyingi: "Akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema."[7]

Alibatizwa ni Yohana katika Mto Yordani. Aliwaita Mitume Kumi na Wawili. Aliwabariki wagonjwa. Aliwafanya vilema kutembea, vipofu kuona, viziwi kusikia. Hata akafufua wafu wakawa hai. Alifunza, akashuhudia, na akatoa mfano kwetu wa kufuatia.

Na kisha huduma ya kimwili ya Mwokozi wa Ulimwenguni ilikaribia kufikia mwisho. Chakula cha mwisho na Mitume wake kilikuwa katika chumba cha juu. Mbele yake kulikuwepo Gethsemane4 na msalaba wa Kalvari.

Hakuna kiumbe kinachoweza kuelewa umuhimu wa kile Kristo alichotufanyia sisi katika Gethsemane. Yeye mwenyewe, baadaye alielezea uzoefu huu: "Mateso ambayo yaliyosababisha Mimi mwenyewe, hata Mungu, mkuu kuliko yote, kutetemeka kwa sababu ya maumivu, na kutoka damu kwenye kila kinyweleo, na kuteseka mwili na roho."[8]

Baada ya mateso ya Gethsemane, sasa ameisha nguvu zote, Akakamatwa kwa mikono ya fujo na jeuri na kupelekwa mbele za Anasi na Kayafa, Pilato10 na Herode. Alituhumiwa na kutukanwa. Kipigo kikali kikazidi kuamusha maumivu ya mwili uliovunjika. Damu ilitiririka kwenye uso wake

pale taji lililotengenezwa kikatili la miba mikali lilipotwekwa kichwani mwake, akidungwa nyusi zake. Na kisha, mara nyingine tena akapelekwa tena kwa Pilato, aliyekubaliana na makelele ya umati uliokasirika: "Msulubishe, msulubishe."[9]

Aliachapwa kwa mjeledi ambao kamba zake nyingi zilifungiliwa vyuma na mifupa yenye ncha ilioshonelewa. Akainuka kutoka kwa ukatili wa kuchapwa, kwa hatua za kujikokota alibeba msalaba wake mwenyewe mpaka alikuwa awezi kuendelea mbele na mwingine akambebea mzigo wake

Mwishowe, kwenye mlima ulioitwa Kalvari, huku wafuasi wasiokuwa na uwezo wakitazama, mwili wake uliojeruhiwa ukapigiliwa kwenye msalaba. Bila huruma alidhihakiwa na kutukanwa na kubezwa. Na bado, akasema kwa sauti, "Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo."[10]

Masaa ya mateso yalipita uhai Wake ulipoisha.1 Kutoka kwa midomo yake iliokauka yalitoka maneno haya, "Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu: na alipokwisha kusema hayo alikata roho."[11]

Shwari na faraja za huruma wa kifo zilimfanya huru kutoka kwa huzuni wa maisha duniani, Akarudi kwenye uwepo wa Baba Yake.

Katika dakika ya mwisho Bwana angegeuka. Lakini hakufanya hivyo. Alijishusha chini ya vitu vyote, ili aweze kuokoa vitu vyote. Mwili Wake usio hai kwa upesi lakini kwa utulivu uliwekwa kwenye kaburi ya kuhazima.

Hakuna neno lolote katika Ukristo lililo na maana kwangu kuliko yale maneno yaliyosemwa na malaika kwa Mariamu Magdalene na yule Mariamu mwengine wakati, wa siku ya kwanza ya wiki, walienda kwenye kaburi kutunza mwili wa Bwana wao. Malaika alisema:

"Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu?

"Hayupo hapa, amefufuka."[12]

Mwokozi wetu akaishi tena. Jambo tukufu, la kufariji na kudhibitisha kati ya mambo yote katika historia ya binadamu lilikuwa limetendeka—ushindi juu ya kifo. Maumivu na mateso ya Gethsemane na Kalvari yalikuwa yamepanguswa. Wokovu wa binadamu ukapatikana. Anguko la Adamu likalipiwa.

Kaburi tupu asubuhi hiyo ya Pasaka ya kwanza lilikuwa jibu la Ayubu, "Kama mtu akifa, ataishi tena?" Kwa wale waliokaribu na sauti ya sauti yangu6 natangaza, kama mtu akifa, ataishi tena. Tunajua, kwani tuna nuru ya ukweli uliofunuliwa.

"Kwani vile kwa binadamu kifo kilikuja, kwa binadamu pia ukaja ufufuko kutoka kwa wafu.

"Kwani kama vile Adamu wote watakufa, hata hivyo katika Kristo wote watafanywa kuwa hai."[13]

Nimesoma—na ninaamni—ushuhuda wa wale waliopata uzoefu wa huzuni wa kusulubishwa kwa Kristo na shangwe ya ufufuko wake. Nimesoma—na naamini—ushuhuda wa wale katika ulimwengu mpya walitembelewa na Bwana aliyefufuka.

Naamini ushuhuda wa mmoja ambaye, katika kipindi hiki, alizungumza na Baba na Mwana katika kichaka sasa kinachojulikana kama Takatifu na ambaye alijitolea maisha, aliufunga ushuhuda huo kwa damu yake. Alitangaza:

"Na sasa baada ya ushuhuda mwingi uliokwisha kutolewa juu yake, huu ni ushuhuda wa mwisho wa zote, ambao tunatoa juu yake: Kwamba yu hai!

"Kwani tulimwona, hata mkono wa kuume wa Mungu; na tukasikia sauti ikitishuhudia kuwa yeye ndiye Mzaliwa wa Pekee wa Baba."[14]

Giza la kifo mara nyingi linaweza kufukuzwa na nuru ya ukweli uliofunuliwa. "Mimi ndimi huu ufufuo, na uzima," alisema Bwana.[15] "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa."[16]

Kwa miaka nimesikia na kusoma ushuhuda mwingi sana zaidi ya kuhesabika, ulioshirikishwa kwangu na watu binafsi ambao walishuhudia uhalisi wa ufufuo na ambao wamepokea, katika masaa mahitaji makuu, imani na ufariji wa Mwokozi.

Nitataja sehemu ya mmoja kama huo. Wiki mbili zilizopita nilipokea barua ya kugusa sana kutoka kwa baba ya watoto saba aliandika kuhusu familia yake na, hasa, mwanawe Jason, ambaye alikuwa mgonjwa alipokuwa wa umri wa miaka 11. Katika miaka michache iliofuatia, ugonjwa wa Jason ulimrudia mara kadhaa. Huyu baba aliongea juu ya mtazamo mzuri wa Jason na uchangamfu wake licha ya changamoto za afya. Jason alipokea Ukuhani wa Haruni akiwa miaka 12 na "kila mara yu tayari kuyapanua majukumu yake kwa ubora, hata kama anajisikia vyema au la" Alipokea tuzo la Eagle Scout alipofika umri wa miaka 14.

Kipindi cha joto kilichopita, sio muda mrefu baada ya maadhimisho

ya kuzaliwa kwake ya miaka 15, alilazwa hospitalini. Katika mojawapo wa matembezi ya kumwona Jason, baba yake alimpata kama amefumga macho. Bila kujua kama Jason alikuwa amelala au anajisikia, alianza kumwongelesha pole pole. "Jason," alisema, "Najua umepitia mengi katika umri wako mdogo na kuwa hali ya sasa ni ngumu sana. Ingawaje una vita vikubwa mbele yako, sitaki kamwe upoteze imani yako katika Yesu Kristo." Alisema alishtuka Jason alipofungua macho na kusema "Kamwe!" Kwa sauti safi, thabiti. Halafu Jason akafunga macho na hakusema tena.

Baba yake aliandika, "Katika tamko rahisi, Jason alionyesha mojawapo wa ushuhuda wa nguvu sana na halisi wa Yesu Kristo ambao nimeshapata kusikia. . . . Kwa tamko lake Kamwe! Lilichorwa kwenye nafsi yangu siku hiyo, moyo wangu ukajazwa na shangwe ambayo Baba Wangu wa Mbinguni amenibariki nayo kuwa baba wa kijana mwema na wa ajabu. . . . Ilikuwa mara mwisho kumsikia akitangaza ushuhuda wake kuhusu Kristo."

Ingawaje familia yake ilikuwa inatarajia kuwa hii ilikuwa kulazwa hosptalini kama kawaida, Jason aliaga dunia katika muda usiozidi wiki mbili. Kaka yake mkubwa na dada walikuwa wanahudumu misheni wakati huo. Kaka yake mwingine, Kyle alikuwa amepokea wito wake wa misheni. Kwa kweli wito ulikuja mapema kuliko vile ilivyotarajiwa na tarehe 5 Agosti, wiki moja kabla Jason kufariki, familia hii ilikusanyika katika chumba cha hospitali ili kwamba barua ya wito wa Kyle ungefunguliwa hapo na kushirikishwa kwa familia yote.

Katika barua yake kwangu, huyu baba aliiweka picha ya Jason katika kitanda cha hospitali, akiwa na kaka yake mkubwa Kyle akisimama kando ya kitanda, akishikilia wito wake wa misheni. Kuna maandishi yaliyoandikwa chini ya picha ile: "Wameitwa kuhudumu misheni zao pamoja—pande zote za pazia."

Kaka ya Jason na dada yake tayari wanahudumu misheni walituma barua za kufariji nyumbani ziweze kushirikishwa kwenye mazishi ya Jason. Dada yake anahudumu Argentina Buenos Aires West Mission, kama sehemu ya barua yake, aliandika: "Najua Yesu Kristo yu hai, na kwa sababu yu hai, sisi sote, pamoja na mpendwa wetu Jason, tutaishi tena pia . . . tunaweza kupata faraja katika elimu ya kweli tuliyonayo kwamba tumefunganishwa pamoja kama familia ya milele. . . . Kama tutafanya juhudi zetu zote kutii na kufanya vyema katika maisha haya, tutamwona [yeye tena]." Akaendelea kwa maandiko, "Maandiko ambayo nimeyapenda sana sasa yanapata maana mpya na umuhimu wakati huu . . . [Kutoka] Ufunuo mlango wa 21, mstari 4: 'Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.' "

Ndugu na dada zangu wapendwa, katika wakati huu wa huzuni, tunaweza kupokea amani kuu kutoka wa maneno ya malaika katika ile asubuhi ya siku ya kwanza ya Pasaka, "Hayupo hapa: amefufuka."[17]

*Amefufuka! Amefufuka!*
*Sema kwa sauti ya shangwe.*
*Ametoweka gereza lake la*
*siku tatu;*
*Acha ulimwengu ufurahie.*
*Mauti yameshindwa,*
*mwanadamu yu huru.*
*Kristo ameshinda Ushindi!*[18]

Kama mmoja wa mashahidi Wake maalumu ulimwenguni leo, hii Jumapili ya Pasaka tukufu, natangaza kwamba hii ni kweli, katika jina Lake takatifu—hata jina la Yesu Kristo, Mwokozi wetu—Amina.

**MUHTASARI**


1. Robert Louis Stevenson, "Requiem," in *An Anthology of Modern Verse,* ed. A. Methuen (1921), 208.
2. James E. Talmage, *Jesus the Christ,* 3rd ed. (1916), 20.
3. Ayubu 14:14.
4. Ona Mwanzo 1:1–27.
5. Ona Ayubu 38:7.
6. Luka 2:52.
7. Matendo ya Mitume 10:38.
8. Mafundisho na Maagano 19:18.
9. Luka 23:21.
10. Luka 23:34.
11. Luka 23:46.
12. Luka 24:5, 6.
13. 1 Wakorintho 15:21, 22.
14. Mafundisho na Maagano 76:22, 23.
15. Yohana 11:25.
16. Yohana 14:27.
17. Mathayo 28:6.
18. "He Is Risen!" *Hymns,* no. 199.


©2010 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimeihifadhiwa. Imechapishwa katika USA. Kiingereza kiliihidhinishwa: 6/09. Tafsiri Ilihidhinishwa: 6/09.
Tafsiri ya *First Presidency Message, May 2010.* Swahill. 09365 743

# Mafundisho ya Wakati Wetu1

Masomo ya Ukuhani wa Melkidezeki na Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama ya Jumapili ya nne yataelekezwa kwa "Mafundisho wa Wakati Wetu." Kila somo linaweza kutayarishwa kutoka kwa hotuba moja au zaidi zilizotolewa katika mkutano mkuu wa hvi majuzi. Marais wa vigingi na wilaya wanaweza kuchagua ni hotuba zipi ambazo zitatumika, au wanaweza kutoa majukumu hayo kwa maaskofu na marais wa matawi. Viongozi wanafaa kusisitiza umuhimu wa kujifunza hotuba hizo hizo kwa ndugu wa Ukuhani wa Melkidezeki na kina dada wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama katika Jumapili sawa sawa.

Wale wanaoudhuria Jumapili ya nne wanahimizwa kusoma na kulete darasani toleo la karibuni la gazeti ya mkutano mkuu.

**Ushawishi wa Matayarisho ya Somo kutoka kwa Hotuba**

Ombeni kwamba Roho Mtakatifu apate kuwa nanyi mnapojifunza na kufunza hotuba hizi. Mnaweza kupendelea kutayarisha kutoka kwa vifaa vingine, lakini hotuba za mkutano mkuu ndio mtalaa uliohidhinishwa. Kazi yenu ni kuwasaidia wengine kujifunza na kuishi injili kama inavyofunzwa katika mkutano mkuu wa majuzi wa Kanisa.


Rejelea hotuba hizi, ukitafuta kanuni na mafundisho yanayoweza kutimiza mahitaji ya wanadarasa. Pia tafuta hadithi, kumbukumbu za maandiko, na matamshi kutoka kwenye hotuba ambayo yatawasaidia kufunza kweli hizi.

Fanya muhtasari wa jinsi ya kufunza kanuni na mafundisho. Muhtasari wako unafaa kujumhisha maswali ambayo yatawasaidia wanadarasa:

- Tafuta kanuni na mafundisho katika hotuba.
- Fikiria kuhusu maana yake.
- Shirikisha ufahamu, mawazo, uzoefu, na ushuhuda.
- Tumieni hizi kanuni na mafundisho katika maisha yenu.

| MIEZI | VIFAA VYA SOMO LA JUMAPILI YA NNE |
|---|---|
| Mei 2010—Oktoba 2010 | Hotuba zilizochapishwa katika *Liahona** ya Mei 2010 |
| Novemba 2010—Aprili 2011 | Hotuba zilizochapishwa katika *Liahona** ya Novemba 2010 |

**Hizi hotuba zipo (katika lugha nyingi) katika conference.lds.org.*



**Na Rais Henry B. Eyring**
Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza

# Wasaidie Njiani Mwao Wakienda Nyumbani

*Tunawasaidia watoto wa Mungu vyema kwa kutoa njia za kujenga imani katika Yesu Kristo na Injili yake ya urejesho wakati wangali wadogo.*

Akina ndugu na dada, Baba wetu wa Mbinguni anataka na anahitaji usaidizi wetu kuwaleta watoto wake wa kiroho nyumbani kwake tena. Nazungumza leo kuhusu vijana ambao tayari wamo katika Kanisa lake la kweli, ambao basi wameanza1 katika njia nyembamba iliyosonga kurejea nyumbani mwao mbinguni. Anawataka wapate nguvu za kiroho mapema za kukaa kwenye njia hii. Na anahitaji usaidizi wetu kuwarejesha upesi ikiwa wataanza kupotoka.

Nilikuwa askofu chipukizi nilipoanza kuona kwa uwazi kwa nini Bwana anatutaka tuwaimarishe watoto wakiwa wachanga na kuwaokoa haraka. Nitawaambia hadithi ya kijana mmoja anayewakilisha wengi ambao nimejaribu kusaidia kwa miaka iliyopita.

Mwanamke aliketi upande mwingine nami katika dawati langu la askofu. Akanieleza kuhusu maisha yake. Alikuwa amebatizwa na kuthibitishwa mshiriki wa Kanisa alipokuwa na miaka minane. Hapakuwa na machozi machoni mwake aliposimulia juu ya zaidi ya miaka 20 iliyofuata, lakini kulikuwa na huzuni kwenye sauti yake. Alisema njia ya mteremko ilianza kwa uamuzi wa kushirikiana na watu ambao alidhani walikuwa wa kusisimua. Alianza kukiuka amri zilizoonekana kwake kwanza kama amri zisizokuwa na umuhimu sana.

Mwanzoni alihisi huzuni kidogo na mchomo1 wa hatia. Lakini ushirikiano na marafiki zake ulimpa hisia ya kupendwa kwa hivyo maamuzi yake ya mara kwa mara ya kutubu yalionekana polepole kupungua kwa umuhimu. Kiwango cha uzito wa amri alizokuwa anavunja kilipoongezeka, ndipo matumaini ya nyumba ya furaha milele yakaonekana kufifia.

Aliketi kinyume yangu katika kile alichokiita mateso. Alitaka nimwokoe kutoka kwa mtego wa dhambi ambayo alijihisi kufungwa kwamo. Lakini njia yake kutoka humo ilikuwa ni kutumia imani katika Yesu Kristo na kuwa na moyo uliovunjika, kutubu na hivyo basi kutakaswa, kubadilishwa na kuimarishwa kupitia kwa Upatanisho wa Bwana. Nilitoa ushuhuda wangu kwamba hiyo iliwezekana. Na ilikuwa, lakini vigumu zaidi ya vile ingelikuwa kutumia imani mapema katika maisha yake katika mwendo wa kurejea nyumbani kwa Mungu na wakati alipoanza kwanza kutangatanga mbali na njia.

Hivyo, tunawasaidia watoto wa Mungu vyema kwa kutoa njia za kujenga imani katika Yesu Kristo na Injili yake iliyorejeshwa wakiwa wachanga. Kisha ni lazima tuwashe tena imani hiyo upesi kabla haijafifia wakitangatanga mbali na njia.

Hivyo, wewe nami tunaweza kutarajia nafasi isiyosita ya kuwasaidia wasafiri kati ya watoto wa Mungu. Mwokozi alituambia kwa nini ingekuwa hivyo alipoeleza safari ya hatari ya kurejea nyumbani kwa wote wa watoto wa kiroho wa Mungu katika ukungu wa dhambi ambao shetani ameweka:

"Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba; kwani mlango ni wazi, na pana ndiyo njia iongozayo kwenye uharibifu na waiendayo ni wengi:

"Kwa sababu mlango umesonga, na njia ni nyembamba iendayo uzimani, nao waipatao ni wachache."[1]

Akiona kimbele mahitaji ya watoto wake, Baba wa Mbinguni mwenye upendo aliweka maagizo na waokoaji kuambaa na njia yao. Alimtuma mwanawe Yesu Kristo kufanya njia yao kuwa salama na inayoonekana. Alimwita kama Nabii wake katika nyakati hizi, Rais Thomas S. Monson. Tangu ujana wake, Rais Monson amefundisha sio tu jinsi ya kukaa katika njia lakini pia jinsi ya kuwaokoa wale ambao wameongozwa kwenye huzuni.

Baba wa Mbinguni ametupangia hali mbalimbali kutuimarisha na ikihitajika, kuongoza wasafiri kwa usalama. Mipango yetu muhimu zaidi na yenye nguvu umo katika familia. Hii ni muhimu kwa sababu familia ina nafasi katika chimbuko la maisha ya mtoto kuthibiti miguu yake kwenye njia kuelekea nyumbani. Wazazi, ndugu na dada na, babu na bibi, shangazi na wajomba wanafanywa kuwa viongozi imara na waokoaji kwa maunganisho ya upendo ambayo ni asilia hasa ya familia.

Familia ina heri katika miaka minane ya kwanza katika maisha ya mtoto. Katika miaka hiyo iliyolindwa, kwa ajili ya upatanisho wa Yesu Kristo, matumizi ya Shetani ya kungu za giza kuficha njia ya kurejea nyumbani hufungwa. Katika miaka hiyo yenye thamani, Bwana huwasaidia familia kwa kuwaita watumishi wa Mafundisho ya Msingi kusaidia kuwaimarisha watoto kiroho. Pia ametoa wenye ukuhani wa Haruni kuhudumia sakramenti. Kwenye hayo maombi ya sakramenti, watoto husikia ahadi kwamba wanaweza kupokea Roho wa Mungu ikiwa watakuwa watiifu kwa amri za Mungu. Kama matokeo, wanaimarishwa kukinza majaribu yatakapokuja na kisha wakati mwingine ujao atakwenda kuwaokoa wengine.

Maaskofu wengi Kanisani wanaongozwa kuwaita watu wenye nguvu zaidi katika Kata kuwahudumia watoto katika Mafundisho ya Msingi. Wanafahamu kwamba ikiwa watoto wataimarishwa, kwa imani na ushuhuda, yaelekea kuwa watahitaji uokoaji kwa kiwango kidogo wakifika umri wa kati ya miaka na. Wanafahamu kwamba msingi imara wa kiroho unaweza kuleta tofauti maishani mwote.

Sote tunaweza kusaidia. Akina bibi, babu na kila mshiriki anayemfahamu mtoto anaweza kusaidia. Haihitaji kuwa na mwito rasmi katika Mafundisho ya Msingi. Wala haizuiwi na umri. Mwanamke mmoja aina hii alikuwa kwenye halmashauri kuu ya Mafundisho ya Kimsingi iliyosaidia kutunga wito wa CTR.

Hakuchoka kamwe kuwahudumia watoto. Alifunza katika Mafundisho ya Msingi katika Kata yake, kwa ombi lake hadi alipokuwa na umri wa karibu miaka 90. Watoto wachanga wangehisi upendo wake kwao. Waliuona mfano wake. Walijifunza kutoka kwake kanuni nyofu za injili ya Yesu Kristo. Zaidi ya yote, kwa ajili ya mfano wake, walijifunza kuhisi na kumtambua Roho mtakatifu. Na walipofanya hivyo, walikuwa tayari katika safari yao kwa imani ya kukataa majaribu. Haielekei wangekuwa na haja ya uokoaji, na walikuwa tayari kwenda kuwaokoa wengine.

Nilijifunza uwezo wa imani nyoofu na maombi wakati watoto wetu walikuwa wachanga. Mwana wetu wa kwanza alikuwa hajabatizwa bado. Wazazi wake, waalimu wa Mafundisho ya Msingi na watumishi wa ukuhani walijaribu kumsaidia kuhisi na kumtambua Roho na kufahamu jinsi ya kupata usaidizi wake.

Siku moja alasiri mke wangu alikuwa amempeleka nyumbani kwa mwanamke ambaye alikuwa anamfundisha kusoma. Mpango wetu ulikuwa kwamba ningemchukua nikiwa njiani kuelekea nyumbani kutoka kazini.

Somo lake lilimalizika mapema kuliko tulivyotarajia. Akawa na hakika kwamba alijua njia ya kwenda nyumbani. Hivyo basi, akaanza kutembea. Baadaye alisema alikuwa na hakika kamili, na alipendelea wazo hili la kuwa pekee yake njiani. Alipokuwa ameenda umbali wa nusu maili (0.8 km), ilianza kushika giza. Akaanza kuhisi kwamba alikuwa bado mbali sana na nyumbani.

Angali anakumbuka kwamba mataa ya magari yalipokuwa yakipita yalitiwa ukungu na machozi yake. Alihisi kama mtoto mchanga wala si mvulana thabiti aliyekuwa ameanza kutembea kwenda nyumbani pekee yake. Alijua kwamba alihitaji msaada. Wazo likamjia kwenye kumbukumbu lake. Alijua kuwa alihitajika kuomba. Hivyo, akaacha barabara na kuelekea kwenye miti ambayo aliona kwa shida gizani. Akapata mahali pa kupiga magoti.

Kupitia kwa vichaka, angesikia sauti zikimwelekea. Watu wawili vijana walikuwa wamemsikia akilia. Walipokaribia, walisema, “tunaweza kukusaidia? Kupitia kwa machozi aliwaambia alikuwa amepotea na alitaka kwenda nyumbani. Wakamuuliza ikiwa alikuwa na nambari ya simu au anwani. Hakuwa nazo. Wakamuuliza ikiwa alijua jina lake. Wakamwongoza hadi mahali karibu walipokuwa wanaishi. Wakapata jina letu la familia katika kitabu cha simu.

Nilipopokea simu nilikimbia kuokoa, nikishukuru kwamba watu wenye huruma walikuwa wamewekwa kuambaa njia yake kwenda nyumbani. Na nimeshukuru daima kwamba alifundishwa kuomba kwa imani kwamba msaada ungefika wakati alipopotea. Imani hiyo imemwongoza kwa usalama na kumletea waokoaji mara nyingi zaidi ya anavyoweza kusimulia.

Bwana ameweka mpangilio wa uokoaji na waokoaji katika ufalme wake. Katika hekima yake, Bwana amewaongoza watumishi wake kuweka baadhi ya mbinu imara zaidi kutuimarisha na kuwaweka waokoaji bora zaidi tunapopita miaka ya ujana.

Mnafahamu kuhusu mipango miwili imara iliyotolewa na Bwana. Mmoja, wa wasichana unaitwa Maendeleo ya Kibinafsi. Mwingine, wa wenye Ukuhani wa Haruni, unaitwa, Wajibu kwa Mungu Tunawahimiza vijana katika uzazi mchanga kuona nguvu zao zisizodhihirika ili kujenga nguvu za kiroho. Na tunawasihi wale wanaowajali vijana kuinuka na kufanya yale Bwana anatuhitaji kufanya ili kuwasaidia. Na kwa vile hali ya baadaye ya Kanisa inawategemea, sote tunawajali.

Mipango hii miwili imeimarishwa lakini dhamira yao haijabadilika. Rais Monson amesema: inatubidi “tujifunze yale lazima kujifunza, tufanye yale lazima kufanywa na kuwa kinachotubidi kuwa.”[2]

Kijitabu cha *Maendeleo ya Kibinafsi* kwa wasichana kinafafanua lengo kwa ajili yao: “Mpango wa Maendeleo ya Kibinafsi hutumia maadili manane ya wasichana kukusaidia kuelewa zaidi wewe ni nani, kwa nini upo hapa duniani, na kile unachofaa kuwa unafanya kama binti wa Mungu kukutayarisha kwa siku utakapoenda hekaluni kufanya maagano.”

Inaendelea kusema wasichana “wataweka ahadi, kuyatimiza na kuripoti maendeleo kwa mzazi au kiongozi.” Inaahidi kwamba “mifano utakayojenga unapofanya kazi ya maendelo ya kibinafsi . . . kama vile maombi, mafunzo ya maandiko, huduma na kuweka shajara itakuwa mazoea ya kibinafsi ya kila siku. Mazoea haya yataimarisha ushuhuda wako na kukusaidia kujfunza na kuzidisha ubora katika maisha yako yote.”[3]

Mpango wa Wajibu kwa Mungu kwa vijana wa Ukuhani wa Haruni umeimarishwa na kulengwa kwenye kiini. Utakuwa ndani ya kitabu kimoja chepesi kwa ajili ya afisi zote tatu za Ukuhani wa haruni. Wavulana na viongozi wao watapokea nakala ya kitabu hiki. Ni kifaa chenye nguvu. Utaimarisha ushuhuda wa wavulana na uhusiano wao na Mungu. Utawasaidia kujifunza kutimiza wajibu wao wa ukuhani. Utaimarisha uhusiano wao na wazazi wao, kati ya wanajamii, na kati ya wavulana na viongozi wao.

Mipango hii miwili inaweka uwajibikaji mkuu katika juhudi za vijana wenyewe. Wanaalikwa kujifunza na kufanya vitu ambavyo vinaweza kuwa changamoto kwa yeyote yule. Ninapotafakari ujana wangu sikumbuki nikiwa na changamoto zaidi hivi. Kwa mara moja nilialikwa kwa mambo magumu kama haya mara kwa mara. Mipango hii inatarajia kuwa na msimamo, juhudi kubwa na ukusanyaji wa mafunzo na uzoefu wa kiroho kwa miaka mingi.

Kwa kutafakari, nilifahamu kuwa vijitabu hivi ni mifano asilia ya imani ya Bwana kwa uzazi mchanga na kwetu sisi sote wanaowapenda. Na nimeona ushahidi kwamba imani hiyo imewekwa pafaapo.

Katika matembezi nilitazama jamii za Ukuhani wa haruni kazini. Nimewaona wavulana wakifuata mifano ya mafundisho, wakifanya mipango ya kufanya yale Mungu anataka kwao, na kuendelea kufanya walijitahidi kufanya na kushirikisha na wengine jinsi walivyobadilika kiroho. Nilipowatazama na kusikiliza, ilionekana dhahiri kwamba akina baba, akina mama, viongozi, marafiki na hata majirani kwenye ushirika waliguswa na roho walipowasikia vijana wakishuhudia waliimarishwa. Vijana waliinuliwa walipotoa ushuhuda na pia wale waliokuwa wakijaribu kuwasaidia kuinuka.

Mpango wa Wasichana unaoo mfano wenye nguvu ya kukuza nguvu za

kiroho kwa wasichana na kutupa nafasi yetu ya kusaidia. Maendeleo ya Kibinafsi huwasaidia Wasichana kujitayarisha kupokea maagano ya hekalu. Wanasaidiwa na mifano ya akina mama, bibi na mwanawake wengine wa haki aliye karibu nao Kanisani. Nimeona jinsi wazazi husaidia binti kufikia malengo yake kwa kuweka maanani na kutambua yale yote mema aliyoyafanya.

Siku chache zilizopita, nilimtazama mama mmoja akisimama na bintiye mdongo walipopokea utambulizi kwa kuwa mifano ya uanauke pambanuzi. Na waliposhiriki nami maana yake kwao, nilihisi idhinisho la Bwana na sote kupewa moyo.

Kwa usaidizi wote tunaoweza kuwapa vijana hawa, lililo kuu zaidi ni kuwaacha wahisi ithibati yetu kwamba wako kwenye njia ya kwenda nyumbani kwa Mungu na kwamba watafaulu. Na tunafanya hivi vyema kwa kwenda nao. Kwa vile njia wakati mwingine una miinuko mikali na miamba, wakati mwingine watafifia moyo na hata kuteguka. Wakati mwingine wanaweza kuchanganyikiwa kuhusu hatima yao na kutangatanga katika kufuata mambo yaliyo na maana kidogo milele. Mipango hii yenye mwongozo wa kiungu hupunguza haya, kwa sababu zitamwongoza kijana kumwalika na kupokea urafiki wa Roho Mtakatifu.

Wasia bora tunaoweza kuwapa vijana ni kwamba wanaweza kurejea kwa Baba wa Mbinguni wanapoongozwa na kukosolewa na Roho wa Mungu. Kwa hivyo tukiwa na hekima tutawahimiza, tutawasifu, na kuwapa mifano yote inayoalika urafiki wa Roho Mtakatifu. Wanapotushirikisha kwa yale wanayoyafanya na kuhisi, ni lazima sisi wenyewe tuwe tumefuzu kwa Roho Mtakatifu. Basi, watahisi katika sifa zetu na tabasamu zetu idhini ya Mungu. Na ikiwa tutahisi kutoa wasia wa kukosoa, watahisi upendo wetu na upendo wa Mungu bali si kemeo na kukataliwa, ambako kutaruhusu shetani kuwaongoza mbali hata zaidi.

Mfano wanaohitaji zaidi kutoka kwetu ni kufanya wanayopaswa kufanya. Tunahitaji kuomba karama za Roho. Tunahitaji kutafakari maandiko na maneno ya manabii wanaoishi. Tunahitaji kufanya mipango ambayo si matamanio tu bali pia ni maagano. Na tunahitaji kutimiza ahadii zetu kwa Mungu. Na tunahitaji kuwainua wengine kwa kuwashirikisha katika baraka za Upatanisho ambazo zimekutujia maishani mwetu.

Na tunahitaji kuonyesha katika maisha yetu mifano isiyogeuka na uaminifu unaoendelea ambao Bwana anatarajia kutoka kwao. Tunapofanya hivi, tutawasaidia kuhisi kutoka kwa Roho hakikisho kwamba ikiwa watashikilia watasikia maneno haya kutoka kwa Mwokozi mwenye upendo na Baba wa Mbinguni ". . . Vema, mtumwa mwema mwaminifu, ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako."[4]

Nashuhudia kwamba Bwana anawapenda na kila mmoja wa watoto wa Mungu. Huu ufalme umerudishwa na funguo za ukuhani kupitia kwa Nabii Joseph Smith. Thomas S. Monson ni Nabii wa Bwana hivi leo. Nawahidi kila mmoja wenu mnapofuata maagizo ya mwongozo wa kiungu katika Kanisa hili la kweli la Yesu Kristo, kwamba vijana wetu nasi wenye kuwasaidia na kuwapenda tunaweza kuwasilishwa salama nyumbani kwetu kwa Baba wa Mbinguni na Mwokozi, kuishi katika familia katika shangwe Milele. Katika jina la Yesu Kristo, amina.

**MUHTASARI**

1. 3 Nefi 14:13–14.
2. Thomas S. Monson, "To Learn, to Do, to Be," *Liahona*, Nov. 2008, 67.2
3. *Young Women Personal Progress* (booklet, 2009), 6.1
4. Mathayo 25:21

©2010 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimeihifadhiwa. Imechapishwa katika USA. Kiingereza kiliihidhinishwa: 6/09. Tafsiri Ilihidhinishwa: 6/09.
Tafsiri ya *Visiting teaching Message, May 2010.* Swahill. 09365 743